# CHUO KIKUU CHA CHUKA

Knowledge is Wealth *(Sapientia divitia est)* Akili ni Mali

## HATI YA UTOAJI HUDUMA KWA WATEJA

**Viwango Vya Huduma**

**Chuo Kikuu cha Chuka kimejitolea kutoa huduma za viwango vya juu. Katika kufanya hivyo, kitazingatia viwango vya juu vya utoaji huduma vifuatavyo:**

| Huduma zinazotolewa | Yanayohitajika | Ada | Muda |
|---|---|---|---|
| Usajili wa wanafunzi | Cheti cha Kipaimara: D (isipokuwa katika taaluma zingine zinazohitaji alama za juu zaidi ) | KSh. 1,000 | Wiki 2 baada ya maombi kupokelewa |
| | Stashahada: C-<br>Shahada ya Kwanza: C+<br>Stashahada ya Juu: Shahada ya kwanza<br>Uzamili:Shahada ya kwanza, daraja ya pili kitengo cha juu au daraja ya pili kitengo cha chini pamoja na tajriba ya miaka miwili ya kufanya kazi<br>Uzamifu:Uzamili | KSh. 2,000 | |
| Utoaji wa vitambulisho vya wanafunzi | Kujisajili katika programu | Kwa mujibu wa mwongozo wa karo | Kwa muda wa wiki 4 baada ya kusajiliwa |
| Ufunzaji | Kujisajili katika programu | Kwa mujibu wa mwongozo wa karo | Kwa mujibu wa ratiba ya semesta/muhula |
| Matokeo ya Mitihani | Kujisajili na kuhudhuria mihadhara | Kwa mujibu wa malipo yaliyoidhinishwa | Matokeo ya mtihani yasiyoidhinishwa yatatolewa wiki 4 baada ya mitihani kukamilika |
| Upataji wa Uzoefu wa Kazi Nyanjani | Kujisajili katika programu | Kwa mujibu wa mwongozo wa karo | Miezi 3 kabla ya kuanza kwa uzoefu nyanjani |
| Usimamizi na Utahini wa Wanafunzi wa Shahada za Juu | Uwasilishaji wa pendekezo, tasnifu na miradi ya utafiti | Kwa mujibu wa mwongozo wa karo | Wiki 4 na 10 baada ya kuwasilisha pendekezo na tasnifu ya mradi wa utafiti mtawalia |
| Ushughulikiaji wa Wateja | Kuidhinishwa baada ya kusajiliwa | Bila malipo | Kwa mujibu wa wakati wa miadi; dakika 3 kwa wale hawana miadi |
| Majibu ya Maulizo ya Kimaandishi | Kauli za wazi za maulizo | Bila malipo | Siku 5 na 7 kwa maulizo rahisi na maulizo changamani mtawalia |
| Majibu ya Malalamiko halali | Malalamiko yaliyoelezwa kwa uwazi na kujitambulisha kwa mlalamishi | Bila malipo | Siku 5 baada ya kutoa malalamiko |
| Malipo kwa wagawaji | Uwasilishaji wa bidhaa/utoaji wa huduma na uwasilishaji wa hati za malipo zifaazo | Bila malipo | Siku 60 |
| Utoaji wa Tenda | Kuwasilisha hati za kuomba tenda | Ada kwa mujibu wa maelekezo kwenye tenda | Siku 14 baada ya kamati ya kutoa tenda kukutana |
| Majibu ya maombi ya kazi | Kutuma maombi | Bila malipo | Miezi 2 |

**Kwa mtu yeyote asiyezingatia viwango hivi au afisa yeyote asiyezingatia utoaji huduma kwa heshima na ubora habari zake ziwasilishwe kwa:**


Mkuu wa chuo, Chuo Kikuu cha Chuka,
S.L.P 109-60400, Chuka, Kenya;
Nambari ya Simu: +254-020-2310512/18
Baruapepe: nairobicampus@chuka.ac.ke
Tovuti: www.chuka.ac.ke

**AMA**

Katibu wa Tume/Mkurugenzi Mkuu Mtendaji,
Tume ya Utawala wa Kisheria, Jumba la West End Towers, Ghorofa ya Pili
S.L.P 20414 – 00200 NAIROBI
Nambari ya Simu: +254-20-270000/2303000/2603765/2441211/8030666
Baruapepe: certificationpc@ombudsman.go.ke
Tovuti: www.ombudsman.go.ke